

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Simu: +255-26- 2323189

Nukushi:255-26-2323088

Barua pepe: ps@moha.go.tz

Tovuti: www.moha.go.tz



Jengo la PSPF

Dodoma Plaza

S.L.P 2916

40483 Dodoma

15 Juni, 2019

**TAASISI ZA KIDINI NA JUMUIYA ZA KIJAMII KUHAKIKIWA
KUANZIA 23 JUNI HADI 02 JULAI, 2019**

Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii na Taasisi za Kidini, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, itafanya uhakiki wa Jumuiya za Kijamii na Taasisi za Kidini nchi nzima. Awamu ya pili ya zoezi la uhakiki itafanyika katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Singida na Manyara tarehe 23 Juni hadi 02 Julai, 2019.

Zoezi la Uhakiki litafanyika katika Kituo cha Uhakiki cha iliyokuwa Ofisi ya Zamani ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

Wakati wa uhakiki nyaraka zifuatazo zinatakiwa kuwasilishwa ikiwemo:-

1. Cheti halisi cha usajili na kivuli cha cheti hicho.
2. Stakabadhi ya mwisho ya malipo ya ada iliyolipwa hivi karibuni.
3. Katiba ya Jumuiya/Taasisi husika iliyopitishwa na Msajili.

4. Barua inayothibitisha uwepo wa Jumuiya/Taasisi hiyo toka kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kata mahali ilipo Ofisi ya Jumuiya/Taasisi husika
5. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka na Taarifa ya Fedha ya Mwaka.

Fomu ya Uhakiki inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa anuani www.moha.go.tz na kwenye Kituo cha Uhakiki.

Taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa kwa mujibu wa ratiba ya eneo husika zitalazimika kwenda Makao Makuu ya Wizara Dodoma kwa ajili ya uhakiki na iwapo zitashindwa kufanyiwa uhakiki kwa muda uliopangwa zitaondolewa kwenye orodha ya Msajili.

Aidha kwa Taasisi za Dini na Jumuiya za Kijamii ambazo hazijasajiliwa zinatakiwa kufika wakati wa zoezi la uhakiki kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kupata usajili.

Pia malipo ya ada yatafanyika wakati wa zoezi la uhakiki kupitia mfumo wa malipo ya Serikali kwa njia ya Kielektroniki (Government Electronic payment Gateway System).

Imetolewa na:


Meja Jenerali Jacob G. Kingu, *ndc*
KATIBU MKUU